

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING`OMBE.
SHULE YA SEKONDARI IGIMA.
KAULI MBIU: *ELIMU NI DIRA***

S. L. P. 714,
NJOMBE.
10/12/2020.

Mawasiliano;

- Barua pepe: igimasecondary17@gmail.com.
- SIMU: 0752- 421549.

Kumb. Na. WDC/S.1604/ISS/JOIN/2020.

Jina la Mwanafunzi:

.....
YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGIMA WILAYA YA WANGING`OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.

1.0: Utangulizi.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kijiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka **2021**. Shule ya Sekondari **Igima** ipo umbali wa km. 27 Mashariki ya makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe. Usafiri wa basi kutoka Njombe mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Njombe mjini. Nauli ni TSH 2,000/. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shulen i kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/01/2021**.

2.0: Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1: Sare za shule.

a) wavulana;

- Suruali **mbili** rangi ya **Damu ya Mzee**. Suruali za kubana hazitaruhusiwa **kabisa**. (angalia kitambaa kilichoambatanishwa)
- Suruali moja rangi ya **Dark Blue** kwa ajili ya wakati wa kazi. **Suruali za kubana hazitaruhusiwa kabisa**.
- Mashati **mawili** (rangi nyeupe mikono mirefu).
- Sweta rangi ya **zambarau** yenye shingo ya "V" (**masweta ya Kenya hayataruhusiwa**)
- Mkanda wa **ngozi** rangi nyeusi
- Soksi **nyeusi** jozi mbili
- Viatu vya ngozi **vyeusi** jozi **mbili** vya **kufunga na kamba**.

b) Wasichana:

- Gauni rangi ya **Damu ya Mzee**, urefu **kuishia kwenye magoti na lisiwe la kubana**. Kitambaa **Na.1.** (**Angalia mchoro ulioambatanishwa**)
- Suruali rangi ya damu ya mzee. (**Suruali na gauni za kubana hazitaruhusiwa kabisa**)
(angalia kitambaa kilichoambatanishwa)
- Sketi moja rangi ya **rangi ya Kijivu ya Kuiva** kwa ajili ya wakati wa kazi.
- Sweta rangi ya **zambarau** yenyne shingo ya “V” (**masweta ya Kenya hayataruhusiwa kabisa**)
- Soksi rangi nyeupe zisipungue jozi mbili.
- Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu.

c) Rangi ya Hijab. (Kwa wanafunzi wa Kiislamu tu)

- Ifanane na Sare za shule. (rangi ya shati)

d) Sare ya Michezo kwa Shule hii ni;

- Raba, T- shirt (fulana) rangi ya njano, bukta rangi ya blue na traki suti rangi ya **blue** kwa ajili ya **wavulana**.
- Raba, T- shirt (fulana) rangi ya njano, Traki suti rangi ya **blue** kwa ajili ya **wasichana**.

2.2: Vifaa Muhimu vya Darasani.

- Daftari kubwa (counter Book three quire) zisizipungue 10
- Kalamu za kutosha
- Mkebe wa hisabati
- Rula ndogo ya sentimeta 30
- Begi dogo la vifaa vya darasani.
- Madaftari madogo 12
- Saa ya mkononi (ya kimulimuli)
- Kamusi (Oxford lugha ya kiingereza kwa kiingereza)
- Four figure (mathematical table) moja.
- Bunda **moja** la karatasi (ream) **A₄** kwa ajili ya mitihani ya kujipima **kila wiki na kila mwezi**

2.3: Chakula cha wanafunzi:

- Mahindi **debe 04** kwa mwaka (debe 02 kwa muhula)
- Maharage **kilo 30** kwa mwaka (kilo 15 kwa muhula)
- Mchele **kilo 20** kwa mwaka (kilo 10 muhula)
- Fedha shilingi **60,000/=** kwa mwaka (30,000/= kwa muhula) zilipwe benki ya NMB AKAUNTI NA. **60601000029**. Jina la Akaunti **IGIMA Sekondari**. Jina la mlipaji aandikwe mwanafunzi kwenye hati ya malipo.
- Aidha kila mwanafuzi alipe shilingi **elfu kumi (10,000/=)** kwenye AKAUNTI tajwa hapo juu kwa ajili ya walimu wa kujitolea masomo ya **sayansi** na **hisabati**.

**NB: HUDUMA YA CHAKULA NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE, KWA SABABU
MWANAFUNZI ATAKUWA SHULENI KUANZIA SAA 12:30 ASUBUHI HADI SAA 12:00 JIONI
SIKU ZOTE ZA MASOMO!**

2.4: Vifaa vya usafi :

- **Wasichana** waje na **fagio** (soft bloom) moja na **kwania** moja.
- **Wavulana jembe** lenye mpini.

3.0: Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii;

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia **mambo ya msingi yafuatayo** ambayo utafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii;

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b) **Mahudhurio mazuri** katika kila shughuri ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f) **Kutunza usafi** wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuvaare sare ya shule **wakati wote** unapotakiwa;
- h) Kuzingatia **ratiba ya shule** wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

3.1: Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule;

- a) wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuoa au kuolewa
- i) Kuwa na mimba
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0: Mambo Mengine Muhimu Yanayopaswa Kukamilishwa na Kuwasilishwa Shulen na Mwanafunzi;

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulen (**Imeambatanishwa**)
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai. (**Imeambatanishwa**)
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule. (**Imeambatanishwa**)

5.0: Tafadhari Soma Kwa Makini Maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII!!

Sanga E. M.

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE
SHULE YA SEKONDARI IGIMA

MKATABA WA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (jina)

Nimesoma na kuelewa kanuni na sheria za shule hii. Kama mwanafunzi nitatumia uwezo wangu wote katika kusoma, kujielimisha na kutii sheria na kanuni za shule. Pia nitashirikiana na Jumuiya ya Shule kwa ujumla , pamoja na wote wenye mamlaka.

Ninaahidi kuwa nitakuwa mwaminifu na sitashiriki kamwe katika vitendo vyovyote kinyume na maadili, pia nitakuwa mstari wa mbele katika kuwafichua wenye nia ya kuvuruga amani na usalama wa shule kwa uwezo wangu wote.

SAHIHI YA MWANAFUNZI:

TAREHE: / /2021

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI:

TAREHE: / /2021

SAHIHI YA MKUU WA SHULE:

TAREHE: / /2021

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING`OMBE.
SHULE YA SEKONDARI IGIMA.
KAULI MBIU: *ELIMU NI DIRA*

Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii;

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia **mambo ya msingi yafuatayo** ambayo utafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni;

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuri ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuvalaa sare ya shule **wakati wote** unapotakiwa;
- h) Kuzingatia **ratiba ya shule** wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

Fuata vyema kanuni zote ufanikiwe kielimu!

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING`OMBE.
SHULE YA SEKONDARI IGIMA.
KAULI MBIU: *ELIMU NI DIRA*

Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule;

- a) wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuoa au kuolewa
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kutaa adhabu kwa makusudi
- l) Kuwa na simu ya mkononi.